**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. PHILIP ISDOR MPANGO, MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WAKATI WA HAFLA NA JUMUIYA YA WATANZANIA WANAOISHI NCHINI MAREKANI.

**18 SEPTEMBA, 2022**

***Mhe. Balozi Liberata R. Mulamula (Mb), Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki;***

***Waheshimiwa Mawaziri Mliopo***

***Bi. Marry Maganga, Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira***

***Waheshimiwa Mabalozi:***

**Waheshimiwa - Viongozi na WanaJumuiya ya Watanzania hapa New York**

***Ndugu Viongozi wengine mnaowakilisha Jumuiya mbalimbali za Watanzania wanaoishi nchini Marekani,***

***Maafisa wa Ubalozi na Watumishi wote wa Serikali mliopo hapa, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana,***

***JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA!***

Awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na fadhili, kwa kutuwezesha kufika siku hii ya leo tukiwa na afya njema. Nawaletea salamu za upendo kutoka nyumbani Tanzania na hususan kutoka kwa Mama yetu mpendwa, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. **Anawasalimu sana!** Aidha, niwashukuru wenyeji wetu kwa kunipatia fursa hii ya kukutana nanyi kwa mara ya kwanza, ndugu zangu mnaoishi hapa Marekani, ili tuweze kufahamiana na kuzungumza machache kuhusu nchi yetu.

Nichukue fursa hii pia, kutoa shukrani zangu kwa Mhe. Balozi Liberata Mulamula (Mb), Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki pamoja na Timu yake ya Wizarani, kwa maandalizi mazuri ya ushiriki wangu katika Mkutano huu wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa.

Kwa namna ya pekee kabisa, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru Viongozi wote wa Jumuiya za Watanzania hapa Marekani, na Diaspora wote wa Tanzania ambao kwa niaba ya wenzenu wengi, mmeona mtenge muda wenu kuja kutusalimia.

***Viongozi na Ndugu zangu Diaspora,***

Kama mnavyofahamu, nimekuja kikazi nchini Marekani ili nimwakilishe Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa. Pamoja na azma hiyo, nimefurahi kupata fursa hii ya kula chakula cha jioni pamoja nanyi ili kuendelea, kukuza na kuimarisha mahusiano katika jamii yetu ya Tanzania.

Nimefahamishwa kuwa wapo Watanzania wengi wanaoisha hapa Marekani katika majimbo mbalimbali lakini wengi wetu hawapo katika umoja wenu huu. Napenda kutoa wito kuwa ni vema mkaendelea kuwa pamoja huku ugenini, kwa kuwa siku zote tunaamini kuwa **Umoja ni Nguvu, Utengano ni Udhaifu!**

Natambua kuwa miongoni mwenu, sehemu kubwa mlikuja nchini Marekani kwa ajili ya kusaka fursa mbalimbali za kiuchumi, elimu na sababu nyinginezo. Wito wangu kwenu nyote ni kuwahimiza muwe na tabia njema na mjiepushe na vitendo vyovyote vya uvunjifu wa sheria mbalimbali. Mchanganyiko mkubwa wa watu wa Mataifa mbalimbali hapa Marekani usije ukawafanya mkajisahau kuwa mpo ugenini na mkaanza kukiuka misingi na desturi zetu ya Ustaarabu wa Kitanzania.

## Mchango wa Diaspora katika Uchumi wa Tanzania

***Viongozi na Ndugu zangu Diaspora;***

Napenda kutumia fursa hii kuwapongeza Diaspora wote wa Tanzania popote Ulimwenguni, kwa namna mnavyounga mkono juhudi za Serikali katika kujiletea maendeleo nyinyi wenyewe na kuchangia maendeleo ya huko nyumbani. Nawapongeza kwa namna ambavyo mmekuwa mkikumbuka ndugu zenu waliopo nyumbani Tanzania, kwa kuwatumia fedha, na hivyo kuzifanya fedha hizo kuingia katika mzunguko wa uchumi wa Taifa letu.

Hivyo, pamoja na pongezi hizi, napenda kutumia fursa hii kuwakumbusha kuwa, pindi mnapotuma fedha zenu nyumbani, basi tumieni mifumo rasmi ya utumaji fedha. Nasema hivi kwa kuwa zipo taarifa kuwa, wengi wenu mnatuma fedha kupitia watu binafsi ambao hawajasajiliwa kufanya shughuli hizo au kupitia mifumo isiyo rasmi. Sasa mnapofanya hivyo, upo uwezekano wa fedha hizo kutofika kwa usalama kwa watu mliowakusudia, na kitendo hicho hutunyima fursa ya kutambua kwa usahihi mchango wenu kupitia fedha mnazotuma nyumbani **(*Remittances*).**

Vilevile, napenda niwapongeze Diaspora wote wa Tanzania hapa Marekani na popote Ulimwenguni, kwa **kuwekeza katika hisa** kupitia Makampuni ya Uwekezaji ya huko nyumbani.

Nimeambiwa kuwa, kupitia UTT – AMIS pekee, hadi mwishoni mwa mwaka 2021 waliweza kuuza kwa Diaspora kiasi cha hisa zenye thamani ya **Shilingi Bilioni 3.9**. Si hayo tuu, hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 2021, Diaspora wa Tanzania kutoka nchi mbalimbali mliweza kununua nyumba nchini Tanzania, zenye thamani ya **Shilingi Bilioni 2.3** kupitia Mradi wa Shirika la Nyumba la Taifa na *Hamidu City Park*, uliopo Kigamboni jijini Dar es Salaam.

***Viongozi na Ndugu zangu Diaspora,***

Vilevile, nawapongeza pia Diaspora wote wa Tanzania pote Ulimwenguni, kwa kuratibu ziara mbalimbali za kitabibu, kutoa misaada ya vifaa tiba na vitabu vyenye thamani ya zaidi ya Dola za Marekani milioni 700 kwa Tanzania Bara na Zanzibar, kuanzia mwaka 2015 hadi 2022.

Hakika, hiyo ni mifano michache tuu inayoonesha mambo mengi mazuri mnayofanya katika kuchangia maendeleo ya sekta mbalimbali nchini Tanzania. Nawaomba muendelee na moyo huo na ninawahakikishia kuwa Serikali inatambua na kuunga mkono juhudi zenu.

## 1. HALI YA UCHUMI

***Ndugu zangu Diaspora,***

Sote tunafahamu uchumi wa nchi nyingi Duniani ulitikiswa sana na janga la UVIKO 19, Tanzania ikiwemo. Kabla ya athari za UVIKO 19, Pato la Taifa lilikuwa linakua kwa wastani wa asilimia 6.5 kwa mwaka na baada ya athari hizo Pato la Taifa lilishuka hadi kufika asilimia 4.8 mwaka 2020. Hata hivyo kwa sasa uchumi unaendelea kuimarika na pato la Taifa lilifikia asilimia 4.9 mwaka 2021. Aidha, mfumuko wa bei umeendelea kubaki katika kiwango kizuri cha tarakimu moja (asilimia 4.6 mwezi Agosti, 2022). Thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Kimarekani imeendelea kuwa imara, pamoja na changamoto mbalimbali ikipungua kwa asilimia ndogo sana. Katika kipindi cha mwezi Julai, 2022, dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa Shilingi 2,315.90 ikilinganishwa na

wastani wa Shilingi 2,316.21 mwezi Agosti, 2022. Utulivu katika soko la fedha za kigeni unatokana na kuimarishwa kwa usimamizi, utekelezaji wa sera thabiti za bajeti na za fedha. Aidha, huduma mbalimbali za msingi zimeendelea kuboreshwa, zikiwemo sekta za afya, elimu, maji na utalii.

Nina imani kuwa nyote mlifuatilia filamu yetu ya *Tanzania Royal Tour.* Napenda kuwaarifu kuwa filamu hiyo imekuwa yenye mafanikio makubwa tangu tuizindue nchini Marekani na baadaye Tanzania. Kwa namna ya pekee, napenda kuwashukuru Mabalozi wa Tanzania waliopo nje ya nchi kwa jitihada zao katika kuhakikisha kuwa Filamu hiyo inatafsiriwa katika lugha mbalimbali, ili iweze kuufikisha ujumbe mzuri wa Utalii uliomo ndani ya filamu hiyo, kwa watu wengi zaidi. Ni dhahiri kuwa, imetusaidia sana kuujulisha Ulimwengu mzima kuhusu utajiri mkubwa wa Vivutio vya Utalii ambavyo nchi yetu imebarikiwa kuwa navyo.

Basi, itoshe tuu kuwahakikishia kuwa pamoja na jitihada za Serikali katika kuimarisha uchumi wetu kupitia Sekta ya Utalii, Uzalishaji, Madini, Uvuvi na nyinginezo, uchumi wetu umeendelea kuimarika siku hadi siku.

## 2. HALI YA SIASA NA USALAMA

***Ndugu zangu Diaspora,***

Kwa upande wa hali ya siasa, Tanzania iko shwari, salama na ina amani tele ya kujivunia. Aidha, Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kujenga mshikamano wa kitaifa kwa kuhakikisha kuwa Vyama vyote vya Siasa nchini Tanzania vinakaa pamoja na kujadili kwa amani, uwazi na uhuru, masuala mbalimbali ili kuendelea kukuza Demokrasia nchini Tanzania pamoja na tunu yetu ya Amani na usalama.

## HITIMISHO

**Waheshimiwa Viongozi na Ndugu zangu Diaspora,**

Kabla sijahitimisha, napenda kutumia fursa hii kusisitiza yafuatayo:

**Kwanza,** muendelee kuchangia maendeleo ya Taifa kwa kuchangamkia fursa mbalimbali za biashara na uwekezaji zinazopatikana nyumbani;

**Pili,** niwakumbushe mtumie mifumo rasmi ya kutuma fedha nchini Tanzania ili fedha mnazotuma nyumbani (remittances) ziweze kuhesabika ipasavyo katika Pato la Taifa (GDP);

**Tatu,** muendelee kushiriki katika kazi endelevu ya kutafuta wawekezaji wa kuwekeza katika miradi mbalimbali inayoendelea nchini Tanzania, na mtusaidie katika kuzitafutia masoko bidhaa mbalimbali zinazozalishwa Tanzania. Fursa mtakazopata, mziwasilishe Ubalozini;

**Nne,** nawaomba muwe mstari wa mbele katika kuvitangaza vivutio vya asili vya Utalii vilivyopo Tanzania Bara na Zanzibar;

**Tano,** uendelee kushirikiana na Ubalozi wa Tanzania hapa Marekani na Serikali yetu, katika kukuza na kuendeleza matumizi zaidi ya Lugha ya Kiswahili, kwa kuanzisha Vituo Rasmi vya Ufundishaji wa Lugha ya Kiswahili, Utamaduni na sanaa mbalimbali za Tanzania. Wakati wa shughuli na maisha yenu hapa Marekani, mjitahidi pia kudumisha mila na desturi kwa kuvaa mavazi ya Kitanzania, kufanya matamasha na maonesho ya utamaduni wa Mtanzania na mambo mengine mazuri;

**Tano,** nawaasa nyote muendelee kuwa Mabalozi wazuri wenye kuitangaza vema Tanzania na muhakikishe wakati wote wanafuata sheria na taratibu zilizowekwa hapa nchini Marekani kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zao mbalimbali. Kumbukeni kuwa vitendo vyovyote vya uvunjifu wa Sheria za nchi hii, vitaharibu heshima yenu binafsi na ya Tanzania kwa ujumla. Hivyo, nawaasa muepuke kujihusisha na matendo ya kihalifu yakiwemo biashara haramu kama vile madawa ya kulevya, ugaidi na mengineyo yatakayoharibu heshima ya Tanzania.

**Sita,** nawasihi kuendelea kushirikiana na Ubalozi wetu, ni vyema mkumbuke kuwa Ubalozi sio kituo cha polisi; bali ni kituo cha kushughulikia masuala ya Diaspora na pia kuwaunganisha Watanzania popote pale walipo kwa madhumuni ya kuleta maendeleo ya ustawi wa jamii yetu.

**Saba,** nawaomba muendelee kuzikumbuka na kuzihudumia familia zenu zilizopo nyumbani. Kwa kufanya hivyo mnashirikiana na Serikali katika kuendeleza na kudumisha ustawi wa familia kwa faida ya Taifa letu.

***Ndugu Wanadiaspora,***

Mwisho kabisa napenda kuwahakikishia kuwa, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaendelea kuwa mstari wa mbele katika kuleta mabadiliko yenye tija kwenye jamii zetu na maendeleo ya nchi yetu kwa ujumla. Vilevile, naamini kuwa kamwe hamtoacha kuwa karibu na nyumbani; na jitihada zenu zitaendelea

kuleta yale mema mliyoyachuma wakati mkiwa huku ughaibuni. Kumbukeni Tanzania itajengwa na Watanzania Wenyewe na ninyi tunawategemea sana katika kuijenga Tanzania.

**Mungu Aibariki Tanzania!**

**Mungu Awabariki Nyote!**

**Asanteni kwa kunisikiliza.**